# Athari za Mtaala wa Umilisi katika Ukuzaji wa Umahiri wa Kuzungumza Kiswahili kwa Wanafunzi wa Shule za Sekondari Nchini Uganda

**Jackline Nasasira, Rhoda Peterson Kidami & Mohamedi Abdallah Ngunguti**
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania*

***Uwasilishaji wa Makala***
Kupokelewa: 2025-06-17
Kurekebishwa: 2025-12-04
Kukubaliwa: 2025-12-16
Kuchapishwa: 2025-12-28

**Maneno Muhimu**
Athari
Maarifa
Mtaala
Umilisi

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Nasasira, J., Kidami, R. P., & Ngunguti, M. A. (2025). Athari za Mtaala wa Umilisi katika Ukuzaji wa Umahiri wa Kuzungumza Kiswahili kwa Wanafunzi wa Shule za Sekondari Nchini Uganda. *Journal of Kiswahili and Other African Languages, 3*(2), 138-146.

Copyright © 2025
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Umahiri wa kuzungumza lugha ni miongoni mwa matokeo yanayotarajiwa kutoka kwa mtu yeyote anayejifunza lugha ya kigeni au lugha ya pili. Mathalani nchini Uganda imebainika kuwa kiwango cha umahiri wa kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari kilikuwa cha chini sana licha ya kufundishwa lugha hiyo kwa kutumia Mtaala wa Maarifa. Utafiti wa awali uliofanywa na watafiti ulibainisha kuwa, kiwango cha umahiri cha wanafunzi kuzungumza lugha ya Kiswahili kimeongezeka tangu kuanza kutumiwa kwa Mtaala wa Umilisi katika ufundishaji mwaka 2020 tofauti na ilivyokuwa chini ya Mtaala wa Maarifa. Kutokana na matokeo hayo, utafiti uliozaa makala haya umetathmini athari za Mtaala wa Umilisi katika ukuzaji wa umahiri wa kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Uganda. Sampuli ya watoataarifa kumi na wawili (12) walimu na ishirini na wanne (24) wanafunzi ilitumika kwenye utafiti huu. Nadharia ya Mawasiliano katika Ufundishaji wa Lugha imetumika katika uchanganuzi wa data za utafiti. Mbinu zilizotumika kukusanya data za utafiti huu ni ushuhudiaji na usaili. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba, athari za Mtaala wa Umilisi katika ukuzaji wa umahiri wa kuzungumza Kiswahili imebainika kuwa mtaala una athari chanya. Athari hizo zipo katika mbinu za ufundishaji, mbinu za ujifunzaji, mawanda ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi husika na mawanda ya ujifunzaji na tathmini.

## Utangulizi

Mtaala[1] wa Umilisi nchini Uganda ni mwendelezo na maboresho ya Mtaala wa Maarifa uliokuwa unatumika awali. Kidega na wenzake (2023) wanaeleza kwamba, mtaala wa shule za sekondari ngazi ya chini nchini Uganda umekuwa wa msingi wa maarifa tofauti na wa umilisi unaohusisha upataji wa ujuzi, maadili na mitazamo. Nchini Uganda serikali imetekeleza Mtaala wa Umilisi ili kuwatayarisha wanafunzi kwa ajili ya soko la ajira.

Katika Mtaala wa Maarifa mwalimu ndiye anayejua kila kitu, haruhusu michango kutoka kwa wanafunzi ambayo inaweza kudhoofisha nafasi yake kama mwalimu. Lengo lake ni kuwafanya wanafunzi kufaulu na kuendelea hadi ngazi inayofuata. Kwa hiyo, wanafunzi hufundishwa tu kile wanachohitaji ili kufaulu mitihani. Mtaala hausisitizi kufanya utafiti na kwa hivyo hautoi maarifa (Kasozi, 2015).

1 Mtaala ni mfumo wa utaratibu wa mafunzo katika kiwango fulani cha kielimu. **Kis.:** mtalaa (BAKITA, 2022:701)

Kulingana na Mtaala wa Ngazi ya Chini wa Shule za Sekondari2 (2019a), Wizara ya Elimu na Michezo kupitia Shirika la Kitaifa la Uandaji wa Mitaala nchini Uganda3 (NCDC), ilifanya mabadiliko ya mtaala wa shule za sekondari ngazi ya chini kwa lengo la kutoa mazingira ya kujifunzia, fursa, mwingiliano, kazi na maigizo. Mambo hayo yanakuza ujifunzaji wa kina kwa kumweka mwanafunzi katikati mwa zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji. Mabadiliko hayo yalitokana na mpango wa sekta ya elimu wa miaka kati ya 2009 na 2018 ulioweka mikakati ya kuboresha elimu ya shule za sekondari.

Mabadiliko hayo yalilenga kutoa mhitimu wa shule ya sekondari ambaye ana umahiri unaohitajika katika karne ya 21, kukuza maadili na mitazamo, kujifunza kwa ufanisi na kupata ujuzi ili kupunguza ukosefu wa ajira miongoni mwa wahitimu (Mtaala wa Ngazi ya Chini wa Shule za Sekondari, 2019a). Badiliko kuu katika Mtaala wa Umilisi ni uhamaji kutoka mtaala wenye msingi katika maarifa hadi ule wenye msingi katika umilisi na stadi. Katika Mtaala wa Umilisi mwanafunzi anahitajika kuwa na uwezo wa kutumia maarifa yake kwa ubunifu. Kiwango cha umilisi hupimwa kupitia uwezo wa kutumia maarifa badala ya kuyapata tu.

Kiswahili nchini Uganda kilifundishwa bila kuzingatia mtaala wowote hadi mwaka wa 2008 ambapo Mtaala wa Maarifa ulianza kutumika (Jjingo na Visser 2017). Kwa hiyo Mtaala wa Maarifa ndio ulitumika kufundishia somo la Kiswahili kuanzia mwaka wa 2008 hadi mwaka wa 2020 ambapo Mtaala wa Umilisi ulianza kutumika.

Kuzungumza ni mchakato wa mwingiliano wa kujenga maana unaohusisha kuzalisha, kupokea na kuchakata taarifa (Brown, 1994; Masinde, Barasa & Mandillah, 2023). Kuzungumza ni mojawapo ya stadi nne za lugha. Stadi zingine ni kusikiliza, kusoma na kuandika (Ur, 1996). Ur (1996) anatambua kuwa stadi ya kuzungumza ni muhimu zaidi kati ya stadi zote nne kwa sababu watu wanaojua lugha fulani kwa kawaida hurejelewa kuwa wazungumzaji wa lugha hiyo. Naye Betul (2015) anaeleza kuwa kuzungumza ni stadi muhimu zaidi kwa wanafunzi kwa sababu ujuzi wa lugha hupimwa kupitia kuzungumza. Kulingana na maelezo ya wataalamu hao (Ur, 1996 na Betul, 2015), ni dhahiri kuwa licha ya kuwa na stadi nne za lugha ambazo ni kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika, stadi ya kuzungumza ni muhimu zaidi. Hivyo, katika mchakato wa kufundisha lugha pamoja na mchakato wa kuchunguza matokeo yaliyofikiwa kutokana na kujifunza lugha fulani, stadi ya kuzungumza inatakiwa kupewa kipaumbele kwani inaweza kuamua mustakabali wa stadi zingine.

Kulingana na tafiti tangulizi (Jjingo, 2011; Jjingo & Visser, 2017), imebainika kuwa umahiri wa kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Uganda umekuwa wa chini licha ya kufundishwa lugha hiyo wakati wa matumizi ya Mtaala wa Maarifa. Kuanzia mwaka wa 2020, Mtaala wa Maarifa ulibadilishwa na Mtaala wa Umilisi ndio unatumika katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji nchini Uganda. Waandishi wa makala haya walifanya utafiti mwaka 2024 kuchunguza umahiri wa wanafunzi kuzungumza Kiswahili baada ya kufundishwa kwa miaka minne kwa kutumia Mtaala wa Umilisi. Utafiti huo umeonesha kuwa, umahiri wa wanafunzi kuzungumza Kiswahili umeongezeka ukilinganisha na hali ilivyokuwa chini ya matumizi ya Mtaala wa Maarifa. Kwa hiyo utafiti huu wa sasa umetathmini athari za Mtaala wa Umilisi katika umahiri wa kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Uganda.

2 Tafsiri ya istilahi ya Kiingereza Lower Secondary School Curriculum
3 Tafsiri ya National Curriculum Developmement Centre

**Nadharia ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Mawasiliano katika Ufundishaji wa Lugha (MUL). Nadharia hii iliasisiwa na wanaisimu Wilkins na Widdowson mwishoni mwa miaka ya 1960 nchini Uingereza (Wilkins, 1976; Widdownson, 1978). Mihimili ya nadharia ya MUL kulingana na waasisi ni minne ambayo ni: Kuamshwa kwa wanafunzi na kuwa na hamu ya kuwasiliana, wanafunzi wanapaswa kuzingatia maudhui ya kile kinachosemwa badala ya sarufi wakati wa kuendeleza shughuli ya ujifunzaji, mwalimu hatamkatisha mwanafunzi kabla sentensi yake haijakamilika na mwalimu darasani ni mwezeshaji. Lengo kuu la nadharia hii ni kukuza uwezo wa kuwasiliana ambapo ujuzi wa miundo ya lugha pia huzingatiwa. Katika muktadha wa kujifunza lugha, mawasiliano yanahusu mambo mengi zaidi ya vipashio vya lugha. Mambo hayo ni kama vile kuanzisha mahusiano, kudumisha mahusiano na kuonesha hisi za mtu.

Nadharia ya MUL imekuwa na mchango mkubwa katika kuchanganua dhima ya mawasiliano katika ufundishaji lugha hatimaye ikawa na waendelezaji tofautitofauti. Waendelezaji wa nadharia hii ni pamoja na Firth (1970), Hymes (1971) na Halliday (1978) kwa mujibu wa Savignon (1983). Wanaisimu hawa wanakubaliana kwamba kujifunza lugha ndiyo kuwasiliana. Firth (1970) ametaja misingi ya utumiaji wa lugha ya kuzungumza kuwa ni namna ya kutumia lugha ya kuzungumza, mwalimu afundishe stadi ya kuzungumza katika muktadha halisi, ufundishaji wa stadi ya kuzungumza uwe kama stadi siyo kama somo na mwalimu awafanye wanafunzi wazungumze mambo yanayotokea kila siku maishani mwao.

Richards (2006) pia ameendeleza nadharia ya MUL na kutaja mihimili 10 ya nadharia hii. Mhimili wa kwanza unaeleza kuwa, ujifunzaji wa lugha ya pili hurahisishwa wakati wanafunzi wanashirikishwa katika mawasiliano yenye maana. Pili, mazoezi ya darasani yenye ufanisi hutoa fursa kwa wanafunzi kujifunza lugha. Tatu, matokeo ya mawasiliano ya maana kutoka kwa wanafunzi huwavutia. Nne, mawasiliano ni mchakato wa jumla ambao huhitaji matumizi ya ujuzi. Tano, ujifunzaji wa lugha huwezeshwa na shughuli zinazohusisha kujifunza kwa kufuata uvumbuzi wa kanuni za msingi za matumizi ya lugha. Sita, ujifunzaji wa lugha ni mchakato wa kiutaratibu unaohusisha matumizi bunifu ya lugha, majaribio na makosa. Ingawa makosa ni jambo la kawaida la kujifunza, lengo kuu la kujifunza lugha ni kuweza kutumia lugha mpya kwa usahihi na ufasaha. Saba, wanafunzi hujifunza lugha kwa viwango tofauti na wana mahitaji na motisha tofauti za ujifunzaji lugha. Nane, ufanisi katika ujifunzaji lugha hutokana na matumizi ya mbinu mwafaka za ujifunzaji lugha na mawasiliano. Tisa, jukumu la mwalimu katika darasa la lugha ni lile la mwezeshaji ambaye hutengeneza hali ya darasani kuwezesha ujifunzaji lugha na kutoa fursa kwa wanafunzi kufanya mazoezi ya matumizi ya lugha. Kumi, darasani wanafunzi hujifunza lugha kupitia kushirikiana na kugawana.

Utafiti huu uliongozwa na mihimili miwili (02) kati ya kumi (10) ya nadharia ya MUL kwa mujibu wa Richards (2006). Mihimili hiyo ni ule wa nane na wa tisa. Mihimili hiyo inaeleza kuwa, ufanisi katika ujifunzaji lugha hutokana na matumizi ya mbinu mwafaka za ujifunzaji lugha na mawasiliano. Hii ni kwa mujibu wa mhimili wa nane. Kwa upande mwingine mhimili wa tisa unaeleza kwamba, jukumu la mwalimu katika darasa la lugha ni lile la mwezeshaji ambaye hutengeneza hali ya darasani kuwezesha ujifunzaji lugha na kutoa fursa kwa wanafunzi kufanya mazoezi ya matumizi ya lugha. Hivyo basi, kwa kuwa masuala ya mtaala hutoa mwongozo wa namna mwalimu anavyofundisha na kufanya tathmini ya kile kinachofundishwa, na utafiti husika ulilenga kutathmini athari za mtaala ambazo zinaweza kuwa chanya au hasi kwenye suala la umahiri wa kuzungumza Kiswahili, mihimili teule ilikuwa faafu katika uchanganuzi wa data za utafiti.

Baada ya utangulizi ulioweka bayana misingi ya kufanyika kwa utafiti uliozaa makala haya pamoja na maelezo ya nadharia iliyotumika katika uchanganuzi wa data, sehemu inayofuata inaweka bayana athari za Mtaala wa Umilisi katika umahiri wa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Uganda kuzungumza lugha ya Kiswahili.

**Athari Chanya za Mtaala wa Umilisi katika Umahiri wa Kuzungumza Kiswahili kwa Wanafunzi wa Shule za Sekondari Nchini Uganda**

Mwongozo wa tathmini hiyo ulikuwa Mtaala wa Umilisi. Hii ni kwa sababu tafiti za awali (taz. Jjingo, 2011; Jjingo na Visser, 2017) zilizofanyika wakati wa matumizi ya Mtaala wa Maarifa zilionesha kwamba wanafunzi hawakuwa na umahiri wa kuzungumza lugha ya Kiswahili. Baada ya kuanzisha Mtaala wa Umilisi nchini Uganda mwaka 2020 watafiti walinuia kufanya utafiti kutathmini umahiri wa kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi lengwa. Tathmini hiyo imeonesha kuwa wanafunzi waliotafitiwa wamepiga hatua katika umahiri wa kuzungumza lugha ya Kiswahili tofauti na ilivyokuwa wakati wa matumizi ya Mtaala wa Maarifa kwenye ufundishaji. Umahiri huo tofauti na awali umeonekana kwa baadhi ya wanafunzi kuweza kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha. Hii inaonesha kuwa kuhama kutoka kwenye Mtaala wa Maarifa kwenda kwenye Mtaala wa Umilisi mwaka 2020 kumekuwa na athari katika umahiri huo.

Kwa ujumla Mtaala wa Umilisi umebainika kuwa na athari chanya katika umahiri wa kuzungumza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Uganda. Athari hizo zimewekwa katika makundi manne ambayo ni mbinu za ufundishaji, mbinu za ujifunzaji, mawanda ya matumizi wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi husika na mawanda ya ujifunzaji na tathmini. Athari hizo zinajadiliwa moja baada ya nyingine katika sehemu inayofuata.

**Athari katika Mbinu za Ufundishaji**

Katika utafiti huu kupitia usaili uliofanyika kwa walimu kuhusu athari za Mtaala wa Umilisi katika umahiri wa wanafunzi wa kuzungumza lugha ya Kiswahili, imebainika kuwa mtaala una athari chanya katika kipengele cha ufundishaji. Hii inaonesha kwamba, ulipoanzishwa Mtaala wa Umilisi mwaka 2020 ulielekeza mbinu bora za ufundishaji lugha ambazo zinachochea mwanafunzi kupata umahiri wa kuzungumza lugha anayojifunza ambapo kwa muktadha wa utafiti huu ni lugha ya Kiswahili. Dondoo lifuatalo ni mojawapo ya maoni aliyoyatoa mwalimu kupitia usaili.

**Dondoo A**

> *Mtaala wa Umilisi umejaa uhalisia. Ukiangalia mpangilio wa mada za Mtaala wa Umilisi, ziliundwa kulingana na maisha anayoyaishi mwanafunzi. Kwa mfano, mada ya kwanza inahusu watu wa nyumbani. Akimaliza kujifunza kuhusu nyumbani anaenda nje ya familia kwa kuangalia jamii, mahali muhimu katika jamii halafu anakuja kwa wanyana na ndege na mada nyingine kwa utaratibu huo. Mpangilio wa mada hizi unamwezesha mwanafunzi kujifunza na kuzungumza Kiswahili kwa utaratibu mno huku akiangalia mambo aliyoyazoea tu maishani. Mtaala wa Umilisi pia umehusisha mbinu kadhaa za kufundishia ambazo zinamwezesha mwanafunzi kujifunza kuzungumza Kiswahili kuliko hali ilivyokuwa katika Mtaala wa Maarifa. Mbinu hizi ni kama vile; nyimbo, majadiliano na uvumbuzi elekezi. Hapa mwanafunzi anafaidika sana kwa sababu anapewa fursa ya kuzungumza Kiswahili.*

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)

Dondoo A hapo juu ni maelezo ya mwalimu mmojawapo akieleza namna Mtaala wa Umilisi ulivyo na athari chanya katika umahiri wa kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Uganda. Kupitia dondoo hilo mwalimu anaeleza kwanza mpangilio wa mada

ambazo zimepangiliwa katika namna ambayo mtiririko wake unamvutia mwanafunzi. Mathalani, mwanafunzi atajifunza watu wa nyumbani na namna ya kuwasiliana nao katika mada ya kwanza. Baada ya hapo atatoka na kuingia kwenye jamii inayomzunguka na kuendelea. Mwalimu pia katika dondoo A hapo juu anaeleza mbinu zinazopaswa kutumika katika ufundishaji kama vile matumizi ya nyimbo na majadiliano. Mbinu hizi pia zimethibitika kuwa na athari chanya katika umahiri wa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Uganda kuzungumza lugha ya Kiswahili.

Mbali na mwalimu aliyetoa maoni yake kuhusu athari chanya za Mtaala wa Umilisi katika umahiri wa kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Uganda, mwalimu mwingine alikuwa na haya ya kusema kupitia dondoo lifuatalo hapa chini.

**Dondoo B**

> *Mtaala wa umilisi katika ufundishaji unahusisha shughuli jumuishi ambazo mwanafunzi anatakiwa kuzifanya kiuhalisia baada ya kumaliza mada fulani. Shughuli jumuishi za mwishoni mwa kila mada kuu ni kama vile kuandika insha. Kupitia uandishi wa insha pia umewasaidia wanafunzi kupata umahiri wa kuzungumza Kiswahili kwa sababu baada ya kuandika insha hizo ninawashirikisha wanafunzi kuzisoma na hapo wanapata msamiati ambao unawasaidia kuzungumza Kiswahili. Pia Mtaala wa Umilisi unamwelekeza mwalimu kuwasimamia wanafunzi kusoma na kukariri mashairi darasani. Shughuli hizi zimewasaidia sana wanafunzi kukuza umahiri wao wa kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa umahiri mkubwa sana.*

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)

Katika Dondoo B hapo juu mwalimu anaeleza namna Mtaala wa Umilisi ulivyo na athari chanya katika umahiri wa kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Uganda. Kupitia dondoo hilo mwalimu anaeleza shughuli ambazo mwanafunzi anatakiwa kuzifanya kila baada ya kukamilisha mada fulani. Shughuli kama uandishi wa insha na mwanafunzi kutakiwa kuzisoma mbele ya darasa zinaongeza umahiri wa mwanafunzi kuzungumza lugha ya Kiswahili. Vilevile suala la kusoma na kukariri mashairi kama ilivyobainishwa na mwalimu kwenye dondoo hapo juu kunaongeza umahiri wa wanafunzi kuzungumza lugha ya Kiswahili.

Ukiangalia hapo juu mbinu zinazotakiwa kutumiwa na walimu wanapofundisha Kiswahili darasani zinaelekea zaidi kumpa mwanafunzi nafasi kubwa ya kushiriki kwenye mchakato kuliko mwalimu. Kutokana na maelezo yaliyotolewa na walimu hapo juu, mwalimu anakuwa tu ni mwelekezaji na mfuatiliaji wa kile kinachotakiwa kufanywa na mwanafunzi. Kwa mfano, mwanafunzi anatakiwa kutunga insha na kuisoma mwenyewe mbele ya darasa badala ya kutungiwa na kusomewa na mwalimu. Utaratibu huu wa ufundishaji unaenda sambamba na madai ya msingi wa MUL uliotumika kuchanganulia data za utafiti huu. Msingi huo unadai kwamba, jukumu la mwalimu katika darasa la lugha ni lile la mwezeshaji ambaye hutengeneza hali ya darasani kuwezesha ujifunzaji lugha na kutoa fursa kwa wanafunzi kufanya mazoezi ya matumizi ya lugha.

**Athari katika Mbinu za Ujifunzaji**

Mbali na athari za Mtaala wa Umilisi kwenye mbinu za ufundishaji, mtaala huu pia umebainika kuwa na athari chanya kwenye mbinu za ujifunzaji. Hii ina maana kwamba, katika suala la ufundishaji mtaala unaelekeza kinachotakiwa kufanywa na mwalimu darasani anapokuwa anafundisha. Kwa upande wa pili mbinu za ujifunzaji zinaelekeza uhusika wa mwanafunzi wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Tutazame yaliyosemwa na mwalimu kwenye dondoo hapa chini wakati wa usaili kuhusu athari chanya za Mtaala wa Umilisi kwa upande wa mbinu za ujifunzaji.

**Dondoo C**

> *Mtaala wa Umilisi umehusisha sana wanafunzi katika mchakato wenyewe wa ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwamba mwanafunzi ndiye anatoa maoni huku mwalimu akimwelekeza tu na kumkosoa panapohitajika. Hivyo, mwanafunzi hupewa nafasi ya kuzungumza Kiswahili. Mtaala wa Umilisi pia unakuza stadi za lugha yaani kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Mtu kuwa na umahiri katika lugha ni lazima ajue stadi zote nne ambazo husisitizwa sana katika Mtaala wa Umilisi. Kila kipindi cha ujifunzaji lazima kinalenga sana kukuza stadi ya kuzungumza.*

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)

Dondoo C hapo juu ni maoni ya mwalimu kuhusu athari chanya za Mtaala wa Umilisi kwenye umahiri wa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Uganda kuzungumza lugha ya Kiswahili. Katika dondoo hilo mwalimu anaeleza kuwa, katika Mtaala wa Umilisi mwanafunzi ndiye anatakiwa kuuhodhi mchakato mzima ambapo mwalimu anakuwa mwelekezaji tu pale inapohitajika kufanya hivyo. Katika mtaala huu mwanafunzi anapewa fursa ya kutoa maoni ya namna anayoona inafaa ili kumwezesha kupata umahiri wa kile anachokusudia kujifunza. Vilevile mwalimu alieleza kuwa, mwanafunzi anatakiwa kumakinikia stadi zote nne za lugha yaani kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika ili apate umahiri toshelevu wa kuzungumza lugha ya Kiswahili.

Yaliyoelezwa na mwalimu kupitia Dondoo C hapo juu yanakubaliana na madai ya misingi miwili ya MUL iliyotumika katika ukusayaji na uchanganuzi wa data za utafiti huu. Mathalani, msingi wa nane unadai kwamba, ufanisi katika ujifunzaji lugha hutokana na matumizi ya mbinu mwafaka za ujifunzaji lugha na mawasiliano. Vilevile mhimili wa tisa unadai kwamba, jukumu la mwalimu katika darasa la lugha ni lile la mwezeshaji ambaye hutengeneza hali ya darasani kuwezesha ujifunzaji lugha na kutoa fursa kwa wanafunzi kufanya mazoezi ya matumizi ya lugha.

**Mawanda ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa Wanafunzi**

Katika kujadili athari chanya za Mtaala wa Umilisi kwenye umahiri wa wanafunzi wa shule za sekondari kuzungumza lugha ya Kiswahili, eneo la mawanda ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi lilionekana kuchagiza umahiri huo. Katika kujadili hili, walimu walieleza kuwa mtaala huu (wa umilisi) unatoa nafasi pana ya wanafunzi kutumia lugha kwenye maeneo tofautitofauti, jambo linalowasaidia kupata umahiri wa kuzungumza Kiswahili. Kupitia Mtaala wa Umilisi wanafunzi wanapewa fursa ya kutumia lugha ya Kiswahili kupitia midahalo yenye mada mtambuka, kuwasilisha hotuba mbalimbali, uimbaji wa nyimbo na matumizi ya semi mbalimbali kwenye miktadha mbalimbali. Kuthibitisha hili, tutazame kile kilichosemwa na mwalimu mmojawapo kupitia dondoo hapa chini.

**Dondoo D**

> *Mtaala wa umilisi unawapa wanafunzi fursa kubwa ya kutumia Kiswahili katika mazingira halisi. Matumizi makubwa ya Kiswahili yanaweza kujidhihirisha kupitia kuwepo kwa midahalo mbalimbali yenye mada tofautitofauti. Kupitia midahalo hiyo, kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki kikamilifu ili kuimarisha umahiri wake wa kuzungumza lugha ya Kiswahili. Kwa kuwa mchakato wa ujifunzaji unawafanya wanafunzi kujihusisha katika somo sana, wanafunzi wengi wameweza kuzungumza Kiswahili. Kila mwanafunzi anaweza kujitambulisha na kusalimiana kwa Kiswahili na mawasiliano mengineyo. Mtaala wa Umilisi unampa fursa mwanafunzi kujifunza hatua kwa hatua*

*kwa sababu lengo kuu ni kujifunza siyo kupita mitihani kama ilivyokuwa katika Mtaala wa Maarifa. Hivyo, mwanafunzi anasoma na kuelewa vizuri bila kubabaishwa na mtihani.*

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)

Mwalimu anaeleza namna mwanafunzi alivyo na fursa ya kutumia Kiswahili kupitia Dondoo D hapo juu. Katika dondoo hapo juu mwalimu anaeleza namna suala la midahalo yenye mada mtambuka inavyowapa wanafunzi fursa ya kutumia Kiswahili kwenye mazingira halisi. Kupitia matumizi mapana ya lugha ya Kiswahili kama yalivyobainishwa na mwalimu, wanafunzi sasa wanaweza kujitambulisha, kusalimiana na mawasiliano mengine kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hii yote inathibitisha namna Mtaala wa Umilisi ulivyo na athari chanya.

Sambamba na uthibitisho uliodhihirika kupitia maelezo ya mwalimu kupitia Dondoo D hapo juu kuhusu athari chanya za Mtaala wa Umilisi katika umahiri wa kuzungumza lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Uganda, vilevile watafiti wakiwa uwandani waliwashuhudia wanafunzi wakiwa wanashiriki kwenye mdahalo mmojawapo. Kwa kutumia mbinu ya ushudiaji, watafiti waliwashuhudia wanafunzi wakishiriki kwenye mdahalo uliokuwa na mada iliyokuwa inasema “Lugha ya Kiswahili iwe ya lazima katika shule za sekondari nchini Uganda”. Katika mdahalo huo watafiti waliwashuhudia wanafunzi wakishiriki kwa kuchangia hoja na kuulizana maswali mbalimbali. Pamoja na kuonesha umahiri wa kuzungumza lugha ya Kiswahili, wanafunzi hao walikuwa na kasoro ndogondogo katika matumizi ya msamiati, miundo na matamshi. Ili kurekebisha kasoro hizo, wanafunzi walirekebishana wao kwa wao na kasoro zingine zilirekebishwa na mwalimu aliyekuwa anasimamia mdahalo huo.

Miongoni mwa hoja zilizotolewa na wanafunzi walioshiriki kwenye mdahalo huo zilidondolewa na watafiti wakati wa ushuhudiaji. Baadhi ya dondoo hizo ni hizi zifuatazo kwenye dondoo E hapa chini.

**Dondoo E**

*Mtoataarifa AA (Aliyekuwa anapinga): Kiswahili haipasi kuwa lugha ya lazima kwa wanafunzi nchini Uganda. Kwa sababu hii siyo lugha ya kwetu ndiyo maana tangu zamani tulikuwa hatufundishwi. Inafaa kuwa ya lazima kwenye nchi kama Tanzania ambako watu wanaongea lugha hiyo tangu wadogo. Pia lugha hii ni ngumu sana tofauti na English.*

*Mtoataarifa BB (Aliyekuwa anaunga hoja): Kupinga matumizi ya lazima ya Kiswahili ni siyo vizuri. Hata kama tumechelewa kuanza kufundishwa Kiswahili, siyo sababu ya kupinga matumizi yake nchini Uganda. Hii ndiyo lugha yetu ya kutuunganisha. Sisi ni bantu na Kiswahili ni bantu language.*

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)

Dondoo E hapo juu linaonesha mjadala walioufanya watoataarifa kwenye mdahalo tajwa. Kupitia mdahalo huo watafiti walishuhudia washiriki wakijieleza kwa Kiswahili na kuonesha umahiri wao katika kuzungumza lugha hiyo. Kupitia mdahalo huo wanafunzi walionesha umahiri mkubwa wa kuzungumza lugha ya Kiswahili licha ya dosari ndogondogo za kimsamiati, muundo na matamshi. Fursa ya midahalo kwa wanafunzi ikiwa ni athari chanya ya Mtaala wa Umilisi imesaidia sana wanafunzi kuwapa fursa ya kutumia lugha ya Kiswahili katika miktadha mbalimbali kwa mada mtambuka. Licha ya kuonesha umahiri wa kuzungumza Kiswahili kupitia mdahalo huo, washiriki walikuwa na dosari ndogondogo kama vile kuchanganya lugha ya Kiingereza walipokuwa wanajenga hoja zao.

Ushiriki wa wanafunzi kwenye mdahalo huo ikiwa ni pamoja na ubunifu wa kujenga hoja na kuziwasilisha kwa umahiri kwa kutumia lugha ya Kiswahili, unakubaliana na msingi wa nadharia ya MUL uliotumika hapa. Msingi huo unadai kwamba jukumu la mwalimu katika darasa la lugha ni lile la mwezeshaji ambaye hutengeneza hali ya darasani kuwezesha ujifunzaji lugha na kutoa fursa kwa wanafunzi kufanya mazoezi ya matumizi ya lugha. Kwa hiyo kupitia mdahalo huo, ilikuwa ni fursa kubwa kwa wanafunzi kufanya mazoezi ya matumizi ya lugha.

**Mawanda ya Ujifunzaji na Tathmini**

Mtaala wa Umilisi vilevile umekuwa na athari chanya katika umahiri wa wanafunzi kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa kuongeza mawanda ya ujifunzaji na tathmini. Kupitia usaili uliofanyika kwa walimu, mwalimu mmojawapo alieleza yafuatayo kuhusu mabadiliko chanya ya Mtaala wa Umilisi ambayo yameongeza umahiri wa wanafunzi kuzungumza lugha ya Kiswahili.

**Dondoo F**

> *Isitoshe, Mtaala wa Umilisi umekuja na mabadiliko katika ufundishaji na tathmini. Kufundisha katika mitaala iliyopita ulikuwa unazingatia uelewa wa mwalimu na tena mwanafunzi kulengwa tu kupata maarifa kutoka kwa mwalimu. Kutathmini (mitihani) kulikuwa kunazingatia vipengele vichache sana ikilinganishwa na mtaala huu wa umilisi. Mtaala huu wa umilisi umekuja na karatasi mbili ambazo zitatathminiwa katika mwisho wa kiwango cha elimu cha O'Level. Karatasi ya pili inazingatia fasihi ya lugha ambayo haikuwemo katika mtaala wa awali. Uchambuzi wa fasihi unajumuisha kuchambua hadithi fupi, mashairi, tamthilia pamoja na novela. Umilisi unaotokana na vipengele vya fasihi umesaidia kukuza umahiri wa wanafunzi hadi kiasi cha kuwa na uwezo wa kutunga tamthilia na mashairi kupitia kuhakiki kazi mbalimbali za kifasihi. Kitambo, haya maswala yalikuwa yanazingatiwa katika kiwango cha A'Level. Jambo hili limesaidia wanafunzi kukuza umahiri wao katika kuzungumza Kiswahili kupitia kuwasilisha baadhi ya vipengele vya kifasihi.*

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)

Kupitia dondoo hapo juu tunaona kwamba Mtaala wa Umilisi umekuja na mabadiliko ambayo yamesaidia kuboresha umahiri wa wanafunzi kuzungumza lugha ya Kiswahili. Kwanza ni suala la kuongeza mawanda ya wanafunzi kusoma. Awali kabla ya Mtaala wa Umilisi, imeelezwa kuwa wanafunzi walifundishwa isimu tu na si fasihi katika daraja la chini la sekondari (O'Level). Lakini baada ya kuanzishwa kwa Mtaala wa Umilisi wanafunzi wanasoma nyanja zote za lugha yaani isimu na fasihi ya Kiswahili. Pili, katika Mtaala wa Umilisi mwanafunzi anatathminiwa katika isimu na fasihi kwa kuwa na mitihani miwili tofauti.

Kwa hiyo, hoja nne zilizozijadiliwa katika kiini cha makala haya ambazo ni mbinu za ufundishaji, mbinu za ujifunzaji, mawanda ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi na mawanda ya ujifunzaji na tathmini zimethibitisha namna Mtaala wa Umilisi ulivyo na athari chanya katika umahiri wa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Uganda kuzungumza lugha ya Kiswahili. Licha ya athari chanya za Mtaala wa Umilisi katika umahiri wa kuzungumza Kiswahili, kuna dosari ndogondogo za wanafunzi katika matumizi ya lugha ya Kiswahili kimsamiati, kimuundo na kimatamshi. Hata hivyo, dosari hizo ni jambo la kawaida katika mchakato wa kujifunza lugha.

Pamoja na athari chanya za Mtaala wa Umilisi katika umahiri wa wanafunzi kuzungumza lugha ya Kiswahili, walimu waliweka wazi baadhi ya vikwazo vinavyoweza kusababisha malengo ya Mtaala wa Umilisi yasifikiwe. Vikwazo hivyo ni kama vile, baadhi ya shule kutokuwa na mwalimu wa

Kiswahili hata mmoja, mlundikano wa wanafunzi kwenye darasa moja, uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kukosekana kwa chombo madhubuti cha kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mtaala husika.

**Hitimisho**

Makala haya ni matokeo ya utafiti uliofanyika kuchunguza umahiri wa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Uganda kuzungumza lugha ya Kiswahili. Matokeo yalionesha kuwa umahiri wa wanafunzi kuzungumza lugha ya Kiswahili uliongezeka baada ya kufundishwa kwa kutumia Mtaala wa Umilisi tofauti na ilivyokuwa awali. Kupitia utafiti uliozaa makala haya, imebainika kuwa Mtaala wa Umilisi una mchango mkubwa katika umahiri huo. Mchango huo umewekwa katika makundi manne ambayo ni mbinu za ufundishaji, mbinu za ujifunzaji, mawanda ya matumizi wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi husika na mawanda ya ujifunzaji na tathmini. Kupitia makala haya, waandishi wanapendekeza kuwa, mahali popote inapofundishwa lugha ni vizuri kutumia mbinu za Mtaala wa Umilisi ili kupata matokeo tarajiwa kwa wakati muafaka.

**Marejeleo**

BAKITA. (2022). *Kamusi Kuu ya Kiswahili (Toleo la 3).* Longhorn Publishers.

Betul, A. S. (2015). "Exploring Anxiety in Speaking Exams and How it Affects Students' Performance". *International Journal of Education and Social Sciences*, Juz. 12 (2): 1-7.

Brown, H. D. (1994). *Principles of Language Learning and Teaching* (Toleo la tano). Pearson Education.

Jjingo, C. (2011). *Language Policy and the Promotion of Kiswahili in Uganda*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Jjingo, C., & Visser, M. (2017). "The Ssenteza Kajubi Legacy: The Promotion of Teaching Kiswahili in Uganda". *Journal of Pan Africa Studies,* Juz, 10 (9): 1-14.

Kasozi, A. B. (2015). "Rethinking our Education System. Part 1. Higher Education". http://www.misr.mak.ac.ug.

Kidega. C, Zheng. S., & Thet, K (2023). "Factors Affecting the Implementation of Competency-Based Curriculum in Lower Secondary Schools in Uganda: A Systematic Literature Review". *North American Academic Research*, Juz. 6 (9): 84 - 102.

Masinde, R., Barasa, D. & Mandillah, L. (2023). Forms of multimodal approaches in the teaching of listening and speaking skills. *Nairobi Journal of Humanities and Social Sciences, 7*(2), 75-90.

National Curriculum Development Centre (2019a). *Lower Secondary Curriculum. Curriculum Framework*. NCDC.

National Curriculum Development Centre (2019b). *Kiswahili Syllabus*. NCDC.

Richards, J. C. (2006). *Communicative Language Teaching Today*: Cambridge University Press.

Savigon, S. J (1983). *Communicative Competence: Theory and Classroom Practice.* Addison-Wesley.

Ur, P. (1996). *A Course in Language Teaching.Practical and Theory*. Cambridge University Press.

Widdowson, H. G. (1978). *Teaching English as Communication*. Oxford University Press.

Wilkins, D. A (1976). *Notional Syllabuses: A taxonomy & its relevance to Foreign Language Curriculum Development.* Oxford University Press.